



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# UFALME WA MUNGU

Leo tutajifunza ufalme wa Mungu, pengine somo muhimu zaidi la Biblia. Maneno ya kwanza ya Yohana Mbatizaji yalikuwa kuhusu ufalme huu: "*Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji, akisema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia*" (Mathayo 3:1,2).

Yalikuwa maneno ya kwanza ya Yesu pia: "*Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia*" (Mathayo 4:17). Mifano saba kati ya mifano ya Yesu katika Mathayo sura ya 13 inajulikana kuwa "Mifano/mafumbo ya Ufalme." Sala ambayo Yesu alifundisha wanafunzi wake inataja ufalme: "*Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni*" (Mathayo 6:9,10).

Mafundisho ya Yesu yaliitwa injili ya ufalme: "Yesu alizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Injili ya ufalme" (Mathayo 9:35). Wanafunzi walitumwa na kuambiwa: "*Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia*" (Mathayo 10:7).

Ingawa somo la ufalme lilikuwa muhimu sana kwa Yesu na wanafunzi wake, ni nadra sana kutajwa katika makanisa na miongoni mwa Wakristo leo. Huenda hilo likawa kwa sababu ya kutoelewa jambo fulani ambalo Yesu alisema: "*Na alipoulizwa na Mafarisayo, Ufalme wa Mungu utakuja lini? Aliwajibu akawaambia, ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema, Tazama, upo huku, au, kule, kwa*

*maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu"* (Luka 17:20,21). Mtazamo wa kawaida umekuwa kwamba ufalme wa Mungu unapaswa kuwa ndani ya mioyo ya watu na si ufalme halisi duniani. Hivyo kuna kazi nyingi ya umishonari ya kusimamisha ufalme wa Mungu katika "mioyo ya wanadamu," kwa kumgeuza kila mtu kuwa Mkristo. Lakini sivyo alivyosema Yesu.

Katika Luka 17:20 Yesu alikuwa akizungumza na Mafarisayo ambao aliwaita hadharani "wanafiki" na "makaburi yaliyopakwa chokaa" (Mathayo 23:27). Hakuwahi kusema kamwe ufalme wa Mungu ungekuwa ndani ya mioyo yao migumu. [1]Hivi ndivyo *Emphatic Diaglott inavyotafsiri* maandishi ya Kigiriki: "Ukuu wa Mungu katikati yenu upo." Ufalme wa Mungu una mfalme na ni Yesu. Ingawa viongozi wa watu hawakumtambua wakati huo, Yesu alisema yeye ndiye mkuu wa ufalme huo ambao kwa kipindi hicho ulikuwa changa bado lakini tayari alikuwa katikati/miongoni mwao.

Ufalme wa Mungu unapaswa kuwa ufalme halisi ambao utafunika na kutawala juu ya dunia yote. Kwa kweli ufalme wa Mungu ulikuwepo juu ya dunia hii muda mrefu uliokwisha kupita, katika bustani ya Edeni. Mungu alimteua Adamu kuwa mfalme juu ya dunia na kusema: "*...Wakatawale...* " (Mwanzo 1:26).

Utawala huo na ufalme ndio unaomaanishwa katika maneno "*na kumvika taji ya utukufu na heshima*" (Zaburi 8:5). Lakini muda mfupi baadaye Mfalme Adamu alipoteza taji yake na ufalme wake. Eva alidanganywa; Adamu alifanya uamuzi wa kufanya alichokifanya Eva. Tokea wakati huo Adamu na kizazi chake wamekuwa watumwa

[1]Maneno kutoka hapa hadi mwisho wa aya hii yaliandikwa na Michael Nekora kuchukua nafasi ya rejeleo la tanbihi ya NIV ambayo haikuweza kuthibitishwa katika Biblia yoyote ya NIV.

wa Shetani, na malaika zake wamewatawala. Shetani alinyang'anya mamlaka na kuanzisha ufalme wake mwenyewe juu ya wanadamu.

Wanadamu pia walianza kuwatawala wanadamu wengine na kuwafanya watumwa. Haya hayakuwa mapenzi ya Mungu kamwe kwa mwanadamu bali aliyaruhusu iwe somo kwao. Hatimaye Mungu alisimamisha ufalme wake wa mfano kati ya watu wake Israeli. Wafalme wa Israeli walisemekana kuketi katika "kiti cha enzi cha Bwana": "*Sulemani akaketi katika kiti cha enzi cha Bwana kama mfalme badala ya Daudi baba yake*" (1 Mambo ya Nyakati 29:23).

Hilo liliendelea hadi kipindi cha Mfalme Sedekia, mfalme wa mwisho wa Yuda, ambaye Bwana alisema hivi kumhusu: "*Na wewe, Ewe mtu mwovu, uliyetiwa jeraha kiasi cha kukuua, mkuu wa Israeli, ambaye siku yako imekuja, wakati uovu utakapokuwa na mwisho; Bwana MUNGU asema hivi; Kiondoe kilemba, ivue taji; haya hayatakuwa tena kama yalivyo; kikweze kilicho chini, kakishushe kilichoinuka. Nitakipindua, nitakipindua, nitakipindua; hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake; nami nitampa*" (Ezekieli 21:25-27)

Kwa kuondolewa kwa Sedekia, ufalme wa mfano wa Mungu katika Israeli uliisha na Wasio Wayahudi wakaanza kuwatawala wakati ambao Biblia inaita "*majira ya Mataifa*" (Luka 21:24). Angalia hasa maneno haya: "*Hata* ***atakapokuja*** *ambaye ni haki yake; nami nitampa yeye*" (Ezekieli 21:27). "Yeye" hurejelea Yesu, yule aliye na haki ya kuwa mfalme katika ufalme wa Mungu, si wakati wa kuja kwake mara ya kwanza, bali katika kuja kwake mara ya pili. Wayahudi walifikiri maneno "*uweza wa kifalme utakuwa mabegani mwake*" (Isaya 9:6) yalimrejelea Masihi katika ujuo wake wa mara ya kwanza, bila kujua kwamba ingetimizwa tu katika ujio wa pili wa Masihi.

Wakristo pia walipoteza uelewa sahihi wa ufalme huo ijapokuwa wanaendelea kuuombea kwa kutumia maneno ya Bwana: "*Ufalme*

*wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni*." Wakristo wametazamia ufalme wa mbinguni pekee wakati Wayahudi wametazamia ufalme wa duniani tu. Lakini kwa kweli ufalme utakuwa wa mbinguni na wa duniani. Malengo matakatifu ya Mungu kwa dunia hii yatatimizwa wakati ufalme wake duniani utakaposimamishwa. Mungu hata alifunua jinsi na wakati ufalme wake utakavyokuja katika ndoto mbili zinazopatikana katika Kitabu cha Danieli.

**Ndoto ya Mfalme Nebukadneza**

"*Hata katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadreza, Nebukadreza aliota ndoto; na roho yake ikafadhaika, usingizi wake ukamwacha. Ndipo mfalme akatoa amri kuwaita waganga, na wachawi, na wasihiri, na Wakaldayo, wapate kumweleza mfalme ndoto zake. Basi wakaingia, wakasimama mbele ya mfalme. Mfalme akawaambia, Nimeota ndoto, na roho yangu imefadhaika hata niijue tafsiri yake. Ndipo hao Wakaldayo wakamwambia mfalme, kwa lugha ya Kiaramu, Ee Mfalme, uishi milele; tuambie sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha tafsiri yake. Mfalme akajibu, akawaambia Wakaldayo, Neno lenyewe limeniondoka; msiponijulisha ile ndoto na tafsiri yake, mtakatwa vipande vipande, na nyumba zenu zitafanywa jaa. Bali kama mkinionyesha ile ndoto na tafsiri yake, nitawapa zawadi na thawabu na heshima nyingi; basi nionyesheni ile ndoto na tafsiri yake. Wakajibu mara ya pili, wakasema, Mfalme na atuambie sisi watumishi wake ile ndoto, nasi tutamwonyesha tafsiri yake. Mfalme akajibu, akasema, Najua hakika ya kuwa mnataka kupata nafasi, kwa sababu mmeona ya kuwa lile neno lenyewe limeniondoka. Lakini msiponijulisha ile ndoto, iko amri moja tu iwapasayo; maana mmepatana kusema maneno ya uongo, na maneno maovu, mbele yangu, hata zamani zitakapobadilika; basi niambieni ile ndoto, nami nitajua ya kuwa mwaweza kunionyesha tafsiri yake. Wakaldayo wakajibu mbele ya mfalme, wakasema, Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme; kwa maana hapana mfalme, wala bwana, wala liwali, aliyetaka neno kama hili kwa mganga, wala kwa mchawi,*

*wala kwa Mkaldayo. Ni neno la ajabu, hili analolitaka mfalme, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili"* (Danieli 2:1-11).

Mfalme Nebukadneza, mfalme wa Babeli, aliota ndoto mbaya sana ambayo ilimsumbua sana akaamka katikati ya usiku na hakupata usingizi tena. Muda si muda alisahau maelezo ya ndoto hiyo, lakini alifadhaika sana akawaita mara moja watu wake wenye hekima, waitwao waganga, wanajimu na wachawi. Waliombwa kumweleza ndoto na kuifasiri. Kwa sababu hakuna awezaye kufanya hivyo, "*Basi kwa hiyo mfalme akaghadhibika sana, akaona hasira nyingi, akatoa amri kuwaangamiza wenye hekima wote wa Babeli*" (Danieli 2:12).

Ingawa walihesabiwa kuwa miongoni mwa watu hao wenye hekima, Danieli na marafiki zake watatu hawakuwapo mfalme alipowapa changamoto viongozi wakuu. Papo hapo Danieli akajibu: "*Ndipo Danieli kwa busara na hadhari akamjibu Arioko, akida wa walinzi wa mfalme, aliyekuwa ametoka ili kuwaua wenye hekima wa Babeli; ....Ndipo Arioko akamwarifu Danieli habari ile. Basi Danieli akaingia, akamwomba mfalme ampe muda, kisha yeye atamwonyesha mfalme tafsiri ile*" (Danieli 2:14-16).

Mfalme amkubalia Danieli ombi lake: "*Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, akawajulisha wenzake neno hilo Hanania, na Mishaeli, na Azaria, kwamba waombe rehema kwa Mungu wa mbinguni kwa habari ya siri hiyo; ili Danieli na wenzake wasiangamie pamoja na wenye hekima wengine wa Babeli. Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika maono ya usiku. Ndipo Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni*" (Danieli 2:17-19)

Danieli na marafiki zake watatu wa Kiebrania waliomba kwanza, kisha Mungu akamfunulia Danieli ndoto hiyo. Danieli akarudi kwa mfalme siku iliyofuata: "*Yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadreza yatakayokuwa siku za mwisho. Ndoto*

*yako, na njozi za kichwa chako kitandani pako, ni hizi; nawe, Ee mfalme, mawazo yako yaliingia moyoni mwako kitandani mwako, yatakayokuwa baadaye; naye afunuaye siri amekujulisha yatakayokuwa. Lakini mimi, sikufunuliwa siri hii kwa hekima niliyo nayo zaidi ya watu wote walio hai, bali ni kwa ajili yao ili kumjulisha mfalme tafsiri hiyo, nawe uyajue mawazo ya moyo wako*" (Danieli 2:28-30).

Kabla ya kueleza jambo lolote, Danieli anatoa sifa na utukufu kwa Mungu na kukazia kwamba hakuwa na hekima zaidi ya wafanyakazi wenzake wakuu zaidi. Aliendelea: "*Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana. Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana, ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha. Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba; miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo. Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote*" (Danieli 2:31-35).

Danieli alimwambia mfalme kwamba aliona sanamu kubwa, ya kutisha kwa sura na ukubwa. Ilitengenezwa kwa metali nne tofauti. Kichwa kilikuwa cha **dhahabu**; mabega, mikono na kifua ilikuwa **fedha**; tumbo na mapaja yalikuwa ya **shaba**; miguu ilikuwa ya **chuma** na nyayo na vidole vya miguu vilikuwa mchanganyiko wa **chuma na udongo-mfinyanzi**.

Kisha jiwe "lisilochongwa kwa mikono ya wanadamu" likaipiga sanamu hiyo na kisha kuponda vipande hivyo mpaka kikawa kama

vumbi; upepo ukavipeperusha. Kisha jiwe hilo likaanza kukua na kuwa "mlima mkubwa na kuijaza dunia yote."

Tafsiri ilifuata: "*Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme, na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na utukufu; na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni na ndege wa angani amewatia mkononi mwako, naye amekumilikisha juu ya hao wote; wewe u kichwa kile cha dhahabu. Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote. Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta*" (Danieli 2:37-40)

Haya yalikuwa maelezo ya milki(falme) nne za ulimwengu ambazo zingetawala ulimwengu mzima kuanzia siku za Danieli. Zilikuwa:

1. Ufalme wa Babeli, K.K 606-538, kichwa cha dhahabu.

2. Ufalme wa Umedi na Uajemi, K.K 538-331, kifua cha fedha na mikono miwili.

3. Ufalme wa Ugiriki, K.K 331-160, tumbo na mapaja ya shaba.

4. Ufalme wa Kirumi, K.K 160 hadi 476 B.K, miguu ya chuma.

Miguu ya chuma iliyochanganyika na udongo-mfinyanzi ilionyesha kwamba ile dola ya Kirumi ya "chuma" iligeuzwa, au kudhoofika: "*Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope. Na kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu yake umevunjika. Na kama vile ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini*

*hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo"* (Danieli 2:41-43)

Chuma safi kilikuwa dola ya Kirumi chini ya uongozi wa kiraia. Udongo unawakilisha mfumo wa kidini chini ya uongozi wa Askofu wa Rumi ambaye alidai mamlaka ya kusimamisha ufalme wa Kristo duniani (Mathayo 6:10). Muungano wa Rumi ya kiraia na Rumi ya kidini ulianza kile ambacho historia inakiita "Himaya Takatifu ya Kirumi," iliyoonyeshwa kwenye miguu na vidole vya miguu ya "chuma kilichochanganyika na udongo-mfinyanzi." Vidole vya miguu ni falme zinazojitegemea kila moja ikidai kuwa ufalme wa Kristo (unaoitwa "Christendom" kwa lugha ya kiingereza) kama vile Milki ya Uingereza, Milki ya Ufaransa, Milki ya Uhispania, n.k.

Udongo-mfinyanzi ni mwamba wa kuiga unaoonyesha kwamba "Falme hizi za Kikristo" ni bandia; wao si wa Mungu wala si wa Kristo. Na hakika zitafikia mwisho wakati ufalme wa kweli wa Mungu utakaposimamishwa: "*Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti"* (Danieli 2:44,45)

Mwamba uliokua na kuijaza dunia yote ni ufalme wa Mungu ulioombwa kwa muda mrefu. Una asili ya mbinguni ("ilikatwa kutoka mlimani bila kazi ya mikono") na umesimamishwa duniani katika "siku za wafalme hao." Ufalme wa Mungu **hautoki** kwa wanadamu bali kwa Mungu. Kwanza unaharibu falme zote za "ulimwengu huu wa uovu wa sasa," kisha "unakuwa mlima mkubwa

na kuijaza dunia yote." Katika ndoto hii Mungu aliwasilisha mfuatano wa falme za ulimwengu ambazo zingetokea moja baada ya nyingine kutoka siku za Danieli hadi nyakati za sasa.

**Ndoto ya Danieli**

"*Katika mwaka wa kwanza wa Belshaza, mfalme wa Babeli, Danieli aliona ndoto, na maono ya kichwa chake, kitandani mwake; basi akaiandika ndoto, akatoa habari ya jumla ya mambo hayo. Danieli akanena, akisema, Naliona katika maono yangu wakati wa usiku; na tazama, hizo pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa*" (Danieli 7:1, 2).

Maono ya Danieli yanaanza na "pepo nne za mbinguni [zinazovuma] juu ya bahari kubwa." "Mbingu" inawakilisha utawala wa kiroho wa dunia na "pepo nne" zinawakilisha njia ambayo kwayo udhibiti au utawala wa kiroho unafanywa juu ya dunia: Kisiasa, Kijamii, Kiuchumi, na Kidini. Ushawishi wa pamoja wa "pepo nne za mbinguni" uko juu ya "bahari kuu" ambayo inawakilisha ulimwengu wa wanadamu katika hali yake ya sasa ya dhambi na mauti: "*Bali waovu ni kama bahari iliyochafuka, ambayo haiwezi kutulia*" (Isaya 57:20). Huu ni Ulimwengu wa Pili kama ulivyokuwepo wakati fulani ambapo unabii huu ulifunuliwa.

Maono hayo yanaendelea: "*Wanyama wakubwa wanne wakapanda kutoka baharini, wa namna mbalimbali*" (Danieli 7:3). Hawa wanyama wanne ni falme nne za ulimwengu ambazo tulijifunza katika Danieli sura ya 2 kwa sababu tunaambiwa: "*Hawa wanyama wakubwa, walio wanne, ni wafalme wanne, watakaotokea katika nchi*" (Danieli 7:17). Ni dola au falme nne za ulimwengu zile zile.

**Mnyama wa 1 — Ufalme wa Babeli**

"*Wa kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai; nikatazama, hata mabawa yake yakafutuka manyoya, akainuliwa katika nchi,*

*akasimamishwa juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa kibinadamu"* (Danieli 7:4).

**"Kama simba"** — ufalme huu una mamlaka kuu, sifa hususa ya Wababeli.

**"Mabawa ya tai"** —hizi zinaashiria vilele kuu vilivyofikiwa na Babeli: "*Kwa maana ukuu wako umekua na kufika mpaka mbinguni*" (Danieli 4:22). Tai huruka juu zaidi kuliko ndege mwingine yeyote. Simba hakutosha kuashiria utukufu mkuu wa Babeli na urefu uliofikia. Ilihitaji "mbawa za tai."

**"Nikatazama mpaka"** —wakati fulani unapita katika historia ya Babeli.

**"Mabawa yakang'olewa(futuka)"** —mamlaka ya kifalme na utukufu wa Nebukadneza viliondolewa: "*Ufalme umeondoka kwako*" (Danieli 4:31).

**"akapewa moyo wa kibinadamu"** —baada ya Nebukadneza kuwa kama mnyama, alinyenyekezwa na kumsifu "Mungu wa mbinguni" (ona Danieli 4:34-37).

**Mnyama wa 2 — Ufalme wa Umedi na Uajemi**

"*Na tazama, mnyama mwingine, wa pili, kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyo hivi, Inuka, ule nyama tele*" (Danieli 7:5).

**"Kama dubu"** — dola la Umedi na Uajemi ilibobea katika mbinu ya kijeshi ya kuzingira na kuwazunguka adui zao, wakizuia usamabazaji wa chakula na kubana maisha kama vile "kabio la dubu" ambalo ni lenye kubana sana kiasi cha kuzuia kupumua.

**“Aliinuliwa upande mmoja”** —kulikuwa na ukosefu wa usawaziko kati ya sehemu mbili za dola hiyo, Waajemi walikuwa wengi zaidi kuliko Wamedi. Katika ndoto ya kwanza, mikono miwili ya sanamu ya Nebukadneza iliwakilisha muungano wa Wamedi na Waajemi.

**“mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake”** —kama vile wanyama wanavyomeza hayawani wengine ndivyo Wamedi na Waajemi walivyoshinda na kuziteketeza falme tatu kabla ya kukamata milki ya ulimwengu. Hizo falme tatu ni: 1) Ufalme wa Misri; 2) Ufalme wa Lidia; 3) Ufalme wa Babeli.

**“Inuka, ule nyama tele”** — maneno hayo yanatoa mamlaka ya kimungu juu ya ufalme wa Umedi na Uajemi kuteketeza ufalme wa Babeli: *“PERESI, ufalme wako umegawanywa, na kupewa Wamedi na Waajemi......”* (Danieli 5:28, 30, 31).

**Mnyama wa 3 — Ufalme wa Uyunani(ugiriki)**

*“Baada ya hayo nikaona, na tazama, mnyama mwingine, kama chui, na juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne ya ndege; huyo mnyama alikuwa na vichwa vinne; naye akapewa mamlaka”* (Danieli 7:6).

**“Kama chui”** — chui, mnyama mwenye kasi zaidi duniani, anaonyesha kasi ambayo Alexanda Mkuu, mfalme mkuu wa Wagiriki, alitumia kuteka ulimwengu wote na kuanzisha ugiriki kuwa ufalme wa ulimwengu.

**“juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne ya ndege”** — Alexandea aliweza kutimiza ushindi wake kupitia majenerali wakuu wanne pekee. "Chui" huyu hakukimbia tu, aliruka asiguse ardhi alipokuwa akiuteka ulimwengu wote.

**"Mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne"** – punde tu ufalme ulipoanzishwa kwamba Alexander alikufa akiwa na umri wa miaka

32. Kwa kuwa hakuwa na mwana, hapakuwa na mrithi. Himaya/dola hiyo iligawanywa katika sehemu nne na kupewa kila mmoja wa majemadari wake: Cassander (Masedonia na Ugiriki), Lysimachus (Asia Ndogo na Thrace), Seleucus Nicator (Mesopotamia na Siria), na Ptolemy (Misri na Palestina).

**Mnyama wa 4 — Ufalme wa Kirumi**

*"Baada ya hayo nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kuogofya, mwenye uwezo mwingi sana; naye alikuwa na meno makubwa ya chuma, alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; naye alikuwa na pembe kumi"* (Danieli 7:7).

**"Ina nguvu kupita kiasi"** —uwezo wa kijeshi wa Rumi ulizidi dola yoyote iliyotangulia mbele yao.

**"Alikuwa na meno makubwa ya chuma"** —hayawani wanatumia meno yao kama silaha za kushambulia kwa hiyo hii inawakilisha "mbinu za vita" za Rumi na hasa, matumizi makibwa ya chuma katika mapigano tofauti na ufalme wowote uliotangulia, na kuwafanya kuwa na nguvu nyingi sana.

**"Alikuwa na pembe kumi"** - ufalme mkubwa wa Kirumi uligawanywa katika sehemu kumi, kila moja chini ya mamlaka ya kifalme. Palestina ilitawaliwa na Herode (ona Luka 23:7; Matendo 25:13).

*"Nikaziangalia sana pembe hizo, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza ziling'olewa na mizizi yake; na tazama, katika pembe hiyo palikuwa na macho kama macho ya mwanadamu; na kinywa cha kunena mambo makuu"* (Danieli 7:8).

**"Nikaziangalia pembe hizo"**— wakati fulani ulipita katika historia ya Dola la Rumi.

**"pembe nyingine ikazuka kati yao, ndogo**" — ufalme mdogo katika Dola la Rumi ukatokea.

**"ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza ziling'olewa**" — maeneo matatu ndani ya Dola la Kirumi (Heruli, Ekstrachate ya Mashariki, na Ostrogothi) yaling'olewa ili kutoa nafasi kwa ile "pembe ndogo," ambayo inaonesha kusimamishwa kwa Askofu wa Rumi ambaye alianzisha ufalme wa aina ya kipekee.

**"Katika pembe hiyo palikuwa na macho kama mwanadamu, na kinywa kilichonena mambo makuu"** — mbinu za hila na werevu zilitumiwa na Askofu wa Rumi kupata mamlaka ndani ya dola la Kirumi hasa kwa kutumia Biblia kama mamlaka ya kusimamisha ufalme wa Mungu duniani.

Hivyo ulizaliwa Upapa. Kila papa alikuwa kama mfalme, akidai ufalme katika mambo ya kiraia na ya kidini tofauti na wafalme (" pembe") wengine. "Pembe ndogo" ni mfumo wa upapa, utawala wa kipekee ambao mwaka 799 BK ulianzisha "Dola Takatifu la Kirumi" ambapo wafalme na watawala wote wa Ulaya wakawa chini ya Papa. Kanisa hili lilitaka kutawala kabla ya ujio wa pili wa Kristo.

Danieli anaendelea: "Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku akaketi" (Danieli 7:9). "Mzee wa Siku" inawakilisha Mungu Baba akikeketi katika hukumu. Katika mstari wa 12 anahukumu hivi: "*Na kwa habari za wale wanyama wengine, walinyang'anywa mamlaka yao…*" Utawala huo akapewa mmoja anayefafanuliwa katika mstari wa 13: "*Mmoja aliye mfano wa Mwana wa Adamu akaja na mawingu ya mbingu, akamjia huyo Mzee wa siku, wakamleta karibu naye.*"

Huyu ndiye Yesu Bwana wetu anayetokea mbele ya Baba wa mbinguni: "*Akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila*

*zote, na mataifa, na lugha zote, wamtumikie; na ufalme wake **hauta**angamizwa*" (Danieli 7:14).

Yesu anapokea "mamlaka na utukufu na ufalme" na mataifa yote yanamtumikia. Ufalme wake utakuwa ufalme wa milele, si ule unaoanza, kisha unaharibiwa na mwingine. Huu unadumu milele. Himaya yake itakuwa ufalme wa Tano wa Ulimwengu mzima: "*Ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu* " (Danieli 7:27).

Huu ni ufalme wa Mungu na unapaswa kushirikiwa na "watakatifu," kanisa la Yesu Kristo katika utimilifu wa ahadi ya Yesu: "*Nami nawawekea ninyi ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi*" (Luka 22:29). Ufalme wa Mungu Yesu anaupokea kutoka kwa Baba, anashiriki na kanisa lake. Hii itokea wakati Yesu atakaporudi kusimamisha ufalme huu duniani (Mathayo 6:10). Sahivi si wakati wa kanisa kutawala; ni wakati ambapo wale wanaotembea katika nyayo za Yesu wanateseka wanapodhihirisha uaminifu wao katika kufikia "mfano wa mwana" "*Tukivumilia, tutatawala pamoja naye; tukimkana, yeye naye atatukana*" (2 Timotheo 2:12). "*Wakizithibitisha nafsi za wanafunzi, na kuwaonya wakae katika imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi*" (Matendo 14:22). "*Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda, nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi*" (Ufunuo 3:21).

Wengi wamekosa kuelewa jambo hili walipofikiri ni sawa kwamba kanisa litawale kabla ya Yesu kurudi. Lakini ufalme halisi wa Mungu unakuja kwenye ujio wa pili wa Yesu wakati wafuasi wake wote waaminifu watapokuwa kama yeye na pamoja naye: "*Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye*" (Mathayo 25:31) Lakini ufalme wa kweli wa Mungu

unakuja katika ujio wa pili wa Yesu. Huo ndio wakati Yesu na kanisa lake watakuja katika utukufu.

Angalia kote ulimwenguni tunamoishi. Hakuna wafalme! Falme zao zote zimetoweka! Tunaishi kwenye mwisho wa wakati uliowekwa kwa falme hizi za ulimwengu. Tunasimama kwenye kizingiti cha Ufalme wa Tano wa Ulimwengu Mzima, ufalme wa Mungu duniani: "*Bwana yu mkono wako wa kuume; Ataseta wafalme, Siku ya ghadhabu yake*" (Zaburi 110:5). "*Ataijaza nchi mizoga*" (Zaburi 110:6).

Kamwe hakujawa na watu wengi zaidi wanaokufa kuliko katika vita vya karne iliyopita: Vita ya Kwanza ya Dunia, Vita ya pili ya Dunia, vita vya Vietnam, vita vya Korea, na vita vya Iran-Iraq. Kumekuwa na mapinduzi katika nchi nyingi ambapo mamia ya maelfu wamekufa. Kwa kweli "mahali pote" (nchi) pamejawa na "mizoga" Kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu kumeanza. Baada ya dunia kupitia tawala za kifalme, Mungu aliruhusu aina nyingine za serikali za majaribio. Hizo ni pamoja na:

**Ukomunisti** —China, Urusi, na baadhi ya nchi za Ulaya zilipata serikali ya kikomunisti. Wote walifikiri kwamba ingeleta amani na ufanisi. Badala yake Urusi iligawanyika vipande vipande na Ukomunisti ukaishia hapo na kwingineko. Hata China inajitahidi kuoanisha ukomunisti na ulaji.

**Ujamaa** —Sawa na ukomunisti, huo pia umethibitika kuwa hautoshi na haufai kitu.

**Demokrasia** —Mtazamo huu maarufu wa kijamii/kisiasa kwa serikali kwa sasa umeonyesha kuwa mbali na kuruhusu kila mtu kuwa na sauti, matokeo yana ushawishi mkubwa wa wale walio na pesa na mamlaka. Kwa hakika maskini hawana sauti.

Aina zote za serikali za wanadamu zitashindwa kwa sababu ufalme wa Mungu ndio jibu pekee. Kama nabii anavyotuambia: "*nacho kile kinachotamaniwa na mataifa yote kitakuja*" (Hagai 2:7). Ufalme wa Mungu utakuwa "kile kinachotamaniwa na mataifa yote" kwa sababu utaleta amani, uzima, na furaha, ambayo ni tamaa ya kila mtu ulimwenguni.

Katika ufalme huo wa utukufu wa Mungu unaokuja...

**Shetani atafungwa na ushawishi wake kuondolewa:** "*Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu, akamtupa katika lile shimo, akamfunga; na kutia muhuri juu yake, asipate tena kuwadanganya mataifa, hata hiyo miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapaswa afunguliwe kwa muda mfupi*" (Ufunuo 20:2,3)

**Macho na masikio ya ufahamu wa watu yatafunguliwa:** "*Na katika siku hiyo viziwi watasikia maneno ya hicho chuo, na macho ya vipofu yataona katika upofu na katika giza*" (Isaya 29:18).

**Ujuzi wa Mungu utajaa dunia nzima:** "*BWANA atakuwa mfalme juu ya dunia yote; siku hiyo kutakuwa na BWANA mmoja, na jina lake moja*" (Zekaria 14:9). "*Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari*." (Habakuki 2:14).

**Mataifa yote yatamtafuta Bwana ili kujifunza kutoka kwake na kumtii:** "*Miisho yote ya dunia itakumbuka na kumrudia BWANA, na kabila zote za mataifa watasujudu mbele zako. Kwa maana ufalme ni wa BWANA, naye ndiye mtawala kati ya mataifa*" (Zaburi 22:27,28). "*Itakuwa katika **siku za mwisho**, mlima wa nyumba ya BWANA utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote yatamiminika huko*" (Isaya 2:2).

**Vita vitakoma:** "*Atahukumu kati ya watu wengi, na kukemea mataifa yenye nguvu yaliyo mbali; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki*

*yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa, wala hawatajifunza vita tena kamwe "* (Mika 4:3).

**Watu watarejea kutoka kwa wafu:** "*Waliokombolewa na BWANA watarudi, watafika Sayuni wakiimba na furaha ya milele juu ya vichwa vyao; watapata furaha na shangwe, huzuni na kuugua zitakimbia*" (Isaya 35:10).

**Hali ya kuzeeka itageuzwa:** "*Nyama ya mwili wake itakuwa laini kuliko ya mtoto; atazirudia siku za ujana wake*" (Ayubu 33:25).

**Hakutakuwa na shida za nyumba:** "*Watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu, na kula matunda yake*" (Isaya 65:21).

**Hakutakuwa na magonjwa wala kuugua:** "*Akaaye ndani yake hatasema, Mimi mgonjwa; watu wakaao ndani yake watasamehewa uovu wao*" (Isaya 33:24).

**Jangwa zitachanua na kuwa bustani yenye rutuba:** "Nafasi kavu itakuwa ziwa la maji, na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji; Maskani ya mbweha walikolala hapo awali, patamea majani, matete na mafunjo" (Isaya 35:7)


**Wanyama wa mwituni watafugwa:** "*Mbwa-mwitu naye atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; na ndama na mwana-simba na kinono pamoja; na mtoto mdogo atawaongoza. Na ng'ombe na dubu watalisha; watoto wao watalala pamoja, na simba atakula majani kama ng'ombe. Na mtoto anyonyaye atacheza kwenye shimo la nyoka, na mtoto aliyeachishwa ataweka mkono wake juu ya pango la nyoka*" (Isaya 11:6-8).

**Kifo hakitakuwapo tena:** "*Mungu atafuta machozi yote katika macho yao; wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita*" (Ufunuo 21:4).

**Ulimwengu utakuwa na amani:** "*Dunia yote inastarehe na kutulia; Hata huanzilisha kuimba*" (Isaya 14:7)

Kwa kweli tunaweza kuombea ufalme huo ujao, kwa bidii zaidi kuliko hapo awali: "*Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe duniani.*"

**-Amina-**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***